**Minutes of meeting of Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**31 May 2008**

**Attendance**
Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Kibwana Mohammad Msiga
Markus Weise
Mussa Alex
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**
Wakati wa wiki Juma na Markus walitembelea Mahenge English Medium school, Kigamboni na Shule ya Tungi, Kigamboni. Tungi ina wapanda baisikeli wanne tu na Mahenge ina 15. Juma pia alitembelea Shule ya Shaban Robert, Upanga tena.

Tulikubali tuwasiliane na HUWATA tena kujua wametembelea shule gani zaidi.

Paulo aliomba nakala ya barua ya shule kwa kiingereza ili awape shule za English Medium na Elaine alisema ataandika.

Tunatayarisha kwa Andrew wa Ben Bikes kuja tarehe 21 Julai kwa wiki moja. Markus anaweza kutumia credit card yake kulipa ndege ya Andrew na UWABA tutarudisha hela zake.

Tulikubali kumwoba Andrew atutumie nakala za karatasi atazitumia kufundisha ili tuone na tuweke kwa kiswahili.

**Ofisi**
Jumanne alisema kwamba mwenye ardhi ambapo tunaweza kujenga ofisi mpya anataka Tsh 40,000 kwa mwezi, maana gharama za ujenzi utakuwa kama kodi za miaka miwili tu. Chaguo zingine ni chumba karibu na Ally Saidi Mohammed (ambayo hainonekani sana kutoka nje) na ofisi nyingine ambayo Dominata alitafuta lakini sasa bahati mbaya imeshachukuliwa. Wakati wa wiki Juma alitafuta ofisi Manzese. Mwenye ofisi, Juma Hassan Chibaya, alijiunga na UWABA na anapanda baisikeli na atapenda kusaidia shirika letu. Yupo tayari kukodisha kwa Tsh 20,000 kwa mwezi, na hatutaanza kulipa mpaka 1 agosti 2008 ambapo kodi ya ofisi ya sasa inamaliza. Ofisi ina ukubwa mara mbili ya ofisi ya sasa na ina dirisha na mlango kubwa na inaonekana sana kutoka barabara. Hasara ni kwamba ipo Manzese wakati watu wamezoea kuja Mabibo lakini ipo karibu na Mabibo na wanachama wa Mabibo walisema haina shida. Ipo karibu sana na nyumbani kwa Juma basi ataweza kufungua ofisi na kusimamia vizuri. Wazi wazi moja ilikuwa kwamba itabomoa katika ujenzi wa barabara ya Morogoro lakini haina shida kwa sababu haipo katika maeneo yatayobomoa. Paa inahitaji marekebisho na Juma Hassan Chibaya alisema atafanya akipata kodi. Ofisi haitumikwi sasa hivi na tunaweza kutumia miezi miwili kupaka rangi na kuandaa.

Baada ya mazungumzo wanachama walikubali kwamba ofisi ya Manzese ni uchaguo mzuri. Tuliandika maktaba pamoja na Elaine ataichapa. Tulikubali Juma atalipa Juma Hassan Chibaya Tsh 40,000 wakati wa wiki kama kodi ili aanze kurekebisha paa.

**Traffic police**
Markus alileta vijitabu tulivyopata wiki tatu iliyopita. Namba za simu kutoa repoti ya kosa na matatizo barabarani ni 0784 304158 (Ilala), 0755 624243 (Kinondoni) na 0754 262636 (Temeke).

Wakati wa wiki Markus alikutana na Bwana Balele wa traffic police. Alisema hairuhusiwi kwa magari kupaki kwenye service roads lakini ngumu kutekeleza. Alisema kuna sheria moja kuhusu barabara tu (Road Traffic Act 1973) na hakuna sheria ndogo. Alipendeka tuandike mawazo na mapendekezo yetu kuhusu vipi serekali inaweza kuangalia matatizo ya wapanda baisikeli.

**TANROADS na barabara mpya**
Wakati wa wiki Markus na Juma waliwapa barau TANROADS Dar es Salaam kuwashukuru kufanya marekebisho maeneo ya Jangwani. Waliongea na meneja waa TANROADS Dar es Salaam Engineer Nyabakari ambaye amefurahi kupokea barua. Alipendekeza UWABA tuandike mawazo na mapendekezo yetu kuhusu vipi kuborehsa mazingira ya wapanda baisikeli.

Markus na Juma walipiga picha za Barabara ya Sam Nujoma na Barabara ya Kilwa. Sam Nujoma kuna njia tatu mahali pengine na njia mbili mahali pengine. Njia moja ni ya magari lakini hatujui njia zingine ni kwa ajili ya watembea kwa miguu, wapanda baisikeli au magari kuingia plot. Barabara ya Kilwa ina njia moja ya ziada pamoja na njia kubwa ya magari. Tulikubali Markus atatoa nakala za picha na ataenda TANROADS kuomba maelezo haya na vipi zinahusika na barua tulizopokea zinazosema kuna njia za baisikeli. Baada ya maelezo tutaweza kuandika mapendekezo yetu.

**Halmashauri la Jiji**
Markus alipewa muda wa kutana na Mama Mlamba lakini hakuwepo ofisini saa ile (labda kwa sababu ya machanganyikio kuhusu saa). Markus aliongea na mkandarasi. Alisema kwamba njia za baisikeli zitalindwa kutoka magari kwa kutumia kerbs. Hajajibu vizuri kuhusu nondo lakini alisema wataiangalia.

**Mapendekezo**
Tuliongea kuhusu mawazo kwa kuwapa TANROADS na traffic police. Mawazo:

- Barabara kubwa ambazo zina service roads
    - Serekali iwe na sheria inayosema lini na vipi magari wanaruhusu au hawaruhusiwi kutumia service roads (mfano kuingia plot, kwenye dharura, kupaki, kupita foleni)
    - Serekali iwe na sheria nzuri kuhusu mwendo mkali, haki ya njia, upande gani wa barabara kutumia
    - Barabara ziwe na alama za barabara ambayo zinaonyesha vizuri sheria hizi
- Barabara zenye njia maalum ya baisikeli
    - Serekali ihakikishe magari yasiingie njia za baisikeli kwenye pande (fereji, miti, kerbs) na yasiingie kwenye sehemu kuingia plots (tumia nondo)
    - Upana wa nondo ziwe pana ya kutosha kutoa sehemu kwa baisikeli za walemavu na wapanda baisikeli lakini siyo pana ya kutosha kwa magari
- Barabara ndogo
    - Tuta kuzuia mwendo mkali ya magari
- zote
    - Mataa ya barabara
    - Miti
- Utekelezaji
    - Wiki ya uamsho kuhusu usalama wa baisikeli na watembea kwa miguu, serekali itangaze sheria na watatekeleza sana wakati wa wiki

**Mambo ya hela**
Juma alitumia Tsh 3,000 kutembelea shule na Tsh 500 kwa photocopy. Juma alipokea Tsh 7,000 ya hela ya guta wakati wa mkutano. Sasa ana Tsh 89,500 ya hela ya UWABA nyumbani.